


Bibilia ya watoto
Inawalettea



Samsoni,
Mtu
Hodari wa
Mungu



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Janie Forest; Alastair Paterson

Imerekebishwa na: Lyn Doerksen

Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya

Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

©2021 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.




Zamani za kale, katika nchi ya Israeli, aliishi mtu aliyeitwa Manoa. Yeye na mke wake hawakuwa na watoto. Siku moja Malaika wa BWANA akamtokea mke wa Manoa. Akasema, "Utakuwa na mtoto wa pekee sana."





Akamwambia mume wake habari hiyo ya ajabu.
Manoa akaomba, "Ee Bwana wangu ... tujie tena.
Tufundishe tutakachotakiwa kumfanyia mtoto."





Malaika akamwambia Manoa kamwe mtoto asikatwe nywele zake, kamwe asinywe kileo, na kamwe asile vyakula fulani. Mungu alimchagua mtoto huyu awe mwamuzi. Awaongoze Israeli.






Hakika
watu wa Mungu walihitaji msaada. Walimuacha
Mungu katika maisha yao, kisha wakaonewa na
maadui zao, Wafilisti. Lakini walipomuomba Mungu
akasikia. Akamtuma huyu mtoto awe mtu hodari
kuliko wote katika dunia nzima.



"Hivyo mwanamke akazaa mtoto na kumuita jina lake Samsoni: na mtoto akakua, na BWANA akambariki. Na roho wa BWANA akaanza kutembea juu yake."

Samsoni akawa hodari sana. Siku moja alipambana na mwana-simba akiwa hana chochote katika mikono yake - na akamuua!





Baadaye, Samsoni akaonja
asali kutoka kwenye nyuki wengi
waliokuwamo kwenye mzoga wa simba.





Akatega kitendawili: "Katika huyo mwenye kula kikatoka chakula, katika huyo mwenye nguvu ukatoka utamu."







Hakuna aliyeweza kukisia maana
yake - lakini mke mpya wa Samsoni,
Mfilisti, akawaambia marafiki zake.
Jambo hili likamkasirisha sana Samsoni.



Samsoni alikasirika zaidi pale wafilisti walipomtoa mke wake kuwa mke wa rafiki yake. Akapanga kulipiza kisasi. Lakini kwa vipi? Kwanza, Samsoni alikamata mbweha 300. Kisha akawafunga mikia yao pamoja, wawili wawili, na akaweka vienge vya moto kati yao.




Kisha Samsoni akawaachia hao mbweha kwenye mashamba ya ngano ya Wafilisti!



Sasa Wafilisti wakataka kulipiza kisasi. Samsoni akaruhusu kukamatwa, kufungwa na kutiwa mikononi kwa Wafilisti ili auawe.



Lakini Roho wa BWANA
akamjia Samsoni. Akazikata
kamba, akaokota mfupa mbichi
wa taya la punda aliyekufa,
na kuua maadui 1000.




Makundi ya Wafilisti yakamtafuta Samsoni. Usiku mmoja, wakamnasa mjini na kufunga milango ya lango la mji. Lakini Samsoni akatoka - akiwa amebeba milango ya lango la mji kwenye mabega yake!





Lakini Samsoni akamuasi Mungu. Mungu alimpa nguvu pale alipomtii. Siku moja, Samsoni alishirikisha siri za nguvu zake kwa Delila, mwanamke mzuri Mfilisti ambaye alikuwa mpelelezi. Akasababisha nywele za Samsoni zinyolewe akiwa amelala.





Kisha maaskari
Wafilisti wakamvamia
Samsoni kwenye
chumba cha kulala
cha Delila. Samsoni
alipambana kwa nguvu
- lakini nguvu zake
zilikuwa zimetoweka.
Maadui zake
wakang'oa macho
yake.







Samsoni akiwa
kipofu na
dhaifu, akawa
mtumwa wa
Wafilisti.
Wakamcheka
na kumdhihaki
mtumishi wa
Mungu.




Wafilisti wakawa na sikukuu. Wakamsifu mungu wao, Dagoni kwa kumtia Samsoni katika mikono yao. Wakanywa na kufurahia kwenye hekalu la Dagoni. Kisha wakamuita Samsoni awafanyie michezo.



Kijana akamleta Samsoni, na kumsaidia kuegemea nguzo zilizoshikilia hekalu. Kulikuwa na Wafilisti 3000 juu ya dari, na wengine wengi hekaluni, wote wakimdhihaki.



Lakini nywele za Samsoni zilikuwa zimeanza kuota akiwa gerezani. Sasa akaomba, "Ee BWANA Mungu, nitie nguvu mara hii tu, ili nipate kujilipiza kisasi kwa ajili ya macho yangu mawili."



Je Mungu angeweza kumtia nguvu tena Samsoni?
Samsoni angeweza kufanya yasiyowezezana?

NDIYO! NDIYO! Pakiwa
pamefurika watu, Samsoni
akazisukuma nguzo imara.
Hekalu la Dagoni
likaanguka na kuua
maelfu ya
Wafilisti
- pamoja na
Samsoni!



Samsoni, Mtu Hodari wa Mungu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Waamuzi 13-16

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

